maeneo ya karibu na barabara za mradi,

- Huduma ya maegesho ya magari,
- Huduma ya matangazo katika miundombinu ya Wakala,
- Uendeshaji wa huduma ya vyoo katika vituo vikuu vya DART.

## 6.0 MAMBO MUHIMU KATIKA UTEKELEZAJI WA MRADI WA DART

- Serikali imejenga miundombinu na inaendelea kujenga miundombinu ya mfumo na kuitunza,
- Kampuni binafsi inamiliki na kuendesha mabasi,
- Malipo yanafanyika kwa uwiano na huduma inayotolewa,
- Utoaji wa huduma mbalimbali ni kwa mikataba na siyo kwa vibali,
- Motisha na adhabu zimewekwa bayana katika mikataba ya huduma ya mabasi na kukusanya nauli,
- Teknolojia ya kisasa inatumika katika usimamizi wa utoaji huduma,
- Utoaji wa huduma za mabasi na mfumo wa ukusanyaji nauli vinafanyika kwa kutumia teknolojia ya kisasa.

## 7.0 MABASI YA MRADI WA DART

Mfumo wa DART unatumia Mabasi makubwa (mita 18) yenye uwezo wa kupakia abiria 129 hadi 140 ikiwa wengi wao wamesimama. Mabasi mengine madogo (mita 12) yana uwezo wa kupakia abiria 80.

## 8.0 FURSA ZA UWEKEZAJI KWENYE MRADI WA DART

- Ujenzi wa miundombinu ya DART,
- Uendeshaji wa Mabasi makubwa na
- Ukusanyaji nauli kwa kutumia teknolojia ya kisasa,
- Utunzaji wa fedha zitokanazo na mfumo,
- Uwekezaji wa pamoja kupitia ushirikiano wa serikali na sekta Binafsi,
- Uendeshaji wa huduma za kijamii kama huduma za hoteli, mgahawa kwenye maeneo ya karibu na barabara za mradi.
- Huduma ya maegesho ya magari,
- Huduma ya matangazo katika miundombinu ya wakala,
- Huduma za kibenki katika mi undo mbinu ya Wakala.

## 9.0 DHAMIRA YA DART

- Kujali wateja,
- Ubunifu,
- Kujituma,
- Ufanisi,
- Ushirikiano na wadau,
- Usalama,
- Hifadhi ya mazingira.


**Mtendaji Mkuu**
Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka
Ubungo Maji, Barabara ya Morogoro,
S.L.P 724, Dar es Salaam, Tanzania,
Simu: +255 22 292 8632-4
Nukushi: +255 22 298 65,
Barua pepe: info@dart.go.tz
Tovuti: www.dart.go.tz

**Mitandao ya kijamii**
Wakala wa Mabasi yaeandayo Haraka
DARTMwendokasi
DARTMwendokasi
DARTTV




**DART**
DAR RAPID TRANSIT

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

## WAKALA WA MABASI YAENDAYO HARAKA

**DAR RAPID TRANSIT (DART)**

# MFUMO MPYA
## WA USAFIRI JIJINI DAR ES SALAAM

## MFUMO MPYA WA USAFIRI WA UMMA JIJINI DAR ES SALAAM UNAOTUMIA NJIA MAALUM NA MABASI MAKUBWA NA MADOGO

### 1:0 DIRA YA DART

Kuwa na usafiri wa umma wa gharama nafuu kwa watumiaji utakaowangizia waendeshaji faida, ukitumia Mabasi ya ujazo mkubwa, ya kisasa yanayokidhi viwango vya ubora wa huduma, hifadhi ya mazingira na utumiaji wa njia maalum ambazo zinafupisha muda wa safari.

### 2.0 MALENGO YA DART

- Kusimamia utekelezaji na uendeshaji wa mfumo wa Mabasi Yaendayo Haraka katika Mkoa wa Dar es Salaam,
- Kuweka mpangilio makini wa matumizi ya barabara kuu na ndogo kwa watumiaji wote ili kupunguza msongamano na
- Kuhakikisha kuwepo kwa Menejimenti ya Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka wenye kuleta tija na ufanisi.

### 3.0 FAIDA ZA MFUMO WA DART

- Kichocheo cha ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi,
- Kupunguza muda wa usafiri kwa asilimia 50%,
- Kupunguza uzalishaji wa hewa ya ukaa (C02),
- Kujali watu wenye mahitaji maalum,
  Fursa za ajira,
- Unazingatia usalama wa abiria,
- Unazingatia ratiba na muda wa safari,
- Huduma haina ubaguzi,
- Unazingatia mahitaji mbalimbali ya makundi maalum,
- Umepunguza msongamano wa magari,
- Umejali watumiaji wengine mfano watembea kwa miguu na waendesha baiskeli
- Umebadilisha mandhari ya jiji la Dar es Salaam na ni kivutio cha utalii.


### 4.0 AWAMU ZA UTEKELEZAJI

Mradi wa DART unatekelezwa katika awamu sita kama ifuatavyo:

- Awamu ya Kwanza ina urefu wa kilometa 20.9 Ikihusisha barabara za Morogoro (Kimar - Kivukoni). Kawawa (Morocco hadi Magomeni), na Msimbazi Fire hadi Kariakoo Gerezani;
- Awamu ya Pili yenye urefu wa kilomita 20.3 inahusisha barabara za Kilwa, Kawawa hadi Mbagala Rangitatu, Gerezani na Chang'ombe;
- Awamu ya Tatu ina jumla ya kilomita 24.2 ikihusisha Barabara ya Nyerere hadi Gongolamboto, Uhuru, Bibi Titi, Azikiwe, Shaurimoyo na Lindi;
- Awamu ya Nne yenye urefu wa kilomita 30. 1 inajumuisha barabara za Sam Nujoma na Bagamoyo hadi Basihaya, Ali Hassan Mwinyi;
- Awamu ya Tano yenye urefu wa kilometa 27.6 inahusisha barabara ya Nelson Mandela, Tabata Segerea hadi Tabata Dampo, Kigogo hadi daraja la Nyerere Barabara ya Kawawa;
- Na awamu ya Sita yenye urefu wa kilomita 26.5 inahusisha barabara ya Mwai Kibaki na barabara mbili za nyongeza kutoka Kimara hadi Kibamba na Mbagala Rangitatu hadi Vikindu.

### RAMANI ZINAZOONYESHA MFUMO MZIMA WA DART WENYE JUMLA YA KILOMITA 149.5




### 5.0 MUUNDO WA KITAASISI KATIKA UTEKELEZAJI WA MFUMO WA DART

- Uendeshaji wa mabasi makubwa na madogo,
- Ukusanyaji nauli kwa kutumia teknolojia ya kisasa,
- Utengenezaji wa tiketi maalum (pre-paid tickets) na kadi janja,
- Utunzaji wa fedha zitokanazo na mfumo,
- Uwekezaji wa pamoja kupitia ushirikiano wa Serikali na Sekta binafsi,
- Uendeshaji wa huduma za kijamii kama huduma za hoteli, mgahawa kwenye mfumo wa DART.